

## USHIRIKIANO

# TMRC yachangia Sh8 mil upasuaji wa watoto JKCI

Michael Matemanga, Mwananchi  
mmatemanga@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Kampuni ya mikopo ya nyumba Tanzania (TMRC) imetoa Sh8 milioni kufanikisha upasuaji wa moyo kwa watoto wanne katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Ofisa mtendaji mkuu wa TMRC, Oscar Mgaya alisema wametoa msaa-da huo baada ya kupata taarifa za uhitaji wa matibabu kwa watoto hao.

“Tulipata taarifa zao baada ya kuona tangazo kwenye televisheni, hivyo tukaona kuna umuhimu wa kufanikisha malipo kwa ajili ya upasuaji wa watoto hawa wanne,” alisema Mgaya.

Kiasi hicho ambacho ni sawa na

Sh2 milioni kwa kila mtoto, alisema ni sehemu ya kampuni hiyo kuihudumia jamii inayofanya nayo biashara.

“Miongoni mwa watoto hawa, wapo wenye ndoto za kuwa wataalamu wa benki, madaktari, marubani au fani nyingine. Taasisi yetu imeona umuhimu wa kufanikisha ndoto zao kwa kuwawezesha matibabu wanayoyahitaji leo,” alisema na kuwataka wadau wengine kujitokeza kusaidia.

Mkurugenzi mtendaji wa JKCI, Profesa Mohamed Janabi alisema taasisi yake imejipanga kupunguza idadi ya wagonjwa wanaokwenda kutibiwa nje ya nchi magonjwa ya moyo badala yake watibiwe nchini kwa gharama nafuu.

Alisema mafanikio yameanza kuonekana kwa kuwa tangu waanze kutoa tiba hiyo mwaka 2008, wamepunguza idadi ya Watanzania wanaotibiwa nje ya nchi.

Profesa Janabi alisema ingawa lengo lilikuwa kutibu watoto 400, lakini tangu Januari hadi sasa, 300 ndiyo wamefanyiwa upasuaji.

Alibainisha kuwa kati ya watoto milioni mbili wanaozaliwa nchini, asilimia moja ambayo ni sawa na 20,000 huwa na tatizo la moyo.

“Wazazi kutozingatia chanjo na lishe bora ni miongoni mwa sababu zinazochangia tatizo hili(moyo),” alisema Profesa Janabi.

## NUKUU

“Tunahamasisha watu kuchangia Sh2 milioni kwa ajili ya matibabu ya watoto wenye hali ngumu na kiasi kingine kinatolewa na Serikali. Kwa wiki hii tutafanya upasuaji kwa watoto 60 na hii ndiyo zawadi ya Sikukuu ya Krismas kutoka kwetu.”

**Profesa Janabi**